JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

TAARIFA KWA UMMA

DCEA YAKAMATA MTANDAO WA KIMATAIFA WA DAWA ZA KULEVYA

Dar es Salaam, Novemba 9, 2026.

Tarehe 6 Novemba 2026, eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ilifanya operesheni na kufanikiwa kukamata jumla ya paketi 299 za dawa za kulevya, zikiwemo paketi 24 za heroin na paketi 275 za methamphetamine. Dawa hizo zilikamatwa zikiwa zimefichwa ndani ya magari mawili aina ya Ford Ranger yenye namba za usajili T.950 ERA na T.417 EJZ, ambayo pia yanashikiliwa kutokana na kuhusishwa na uhalifu huo. watuhumiwa wanne (4) walikamatwa katika operesheni hiyo.

Watuhumiwa hao ni JUMA SLAATI KISOMEKO (36), raia wa Uganda, dereva na mkazi wa Piji, nchini Uganda; ISSA SAID NASSORO (34), mfanyabiashara; IBRAHIM SAID CHEMBELA (30), dereva; na MOHAMED ALLY SHEMTUU (45), dereva. Watuhumiwa watatu wa mwisho ni wakazi wa Tabata, jijini Dar es Salaam.

Baada ya kukamatwa na kuhojiwa, watuhumiwa hao wameeleza kuwa, dawa hizo walizichukua Mombasa, Kenya na kuzisafirisha kuingia Tanzania kupitia mpaka wa Horohoro mkoani Tanga. Kutokana na maelezo hayo, DCEA iliwasiliana na mamlaka husika nchini Kenya na kushirikiana kiutendaji kwa lengo la kubaini chanzo, eneo lililotumika kuhifadhi dawa hizo, pamoja na kuwabaini wahusika wengine wa mtandao huo.

Kupitia ushirikiano huo, tarehe 7 Novemba, 2026, DCEA na Kitengo cha Kitaifa cha Kudhibiti Dawa za Kulevya nchini Kenya (NANB) zilifanikisha ukamataji wa paketi 454 za dawa ya kulevya aina ya methamphetamine kufuatia operesheni iliyofanyika eneo la Kwale jijini Mombasa, Kenya.

Katika operesheni hiyo, watuhumiwa wengine watatu walikamatwa. Watuhumiwa hao ni SALEH KHAMIS BASELEMAN (45), maarufu kwa jina la MBWIGA, raia wa Tanzania, mfanyabiashara na mkazi wa Mombasa, nchini Kenya; SEIF SAID HAMAD (54), maarufu kwa jina la BABU SEIF, raia wa Tanzania, mvuvi na mkazi wa Kinondo, Mombasa, nchini Kenya; na ZURAICAH AHMED HUSSEIN (25), raia wa Uganda, mfanyabiashara na mkazi wa Shirazi, Mombasa, nchini Kenya.

Taratibu za kisheria kati ya Tanzania na Kenya zinaendelea ili kuhakikisha watuhumiwa wote wanafikishwa mbele ya vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

Baadhi ya watuhumiwa waliokamatwa ni vinara wa mtandao wa kimataifa wa usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya wanaofanya shughuli zao katika nchi mbalimbali, zikiwemo Afghanistan, Afrika Kusini, Msumbiji, Zambia, Malawi, Uganda, Kenya, Tanzania na Dubai.

08 Barabara ya Kivukoni, S.L.P. 80327, 11486 Dar es Salaam; Simu: +255 22 211 3754/57;
Nukushi: +255 22 211 3752; Barua pepe: cg@dcea.go.tz; Tovuti: www.dcea.go.tz

Mathalani, SALEH KHAMIS BASELEMAN, maarufu kama MBWIGA, anadaiwa kununua dawa za kulevya moja kwa moja kutoka nchini Afghanstan na kuzisafirisha kwa njia ya bahari mpaka katika fukwe za Mombasa, nchini Kenya, kabla ya kuzisambaza katika nchi mbalimbali, ikiwemo Tanzania.

Kadhalika anahusishwa na ukamataji wa dawa za kulevya tani 3.5 zilizokamatwa na DCEA mwezi Desemba mwaka 2023 eneo la Kigamboni, jijini Dar es Salaam na mkoni Iringa.

Mafanikio yaliyopatikana katika operesheni hii yanaonesha umuhimu wa ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika kukabiliana na dawa za kulevya Duniani. Hivyo, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inatoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa kuhusu viashiria vya uwepo wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Kamishna

Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA
NA DAWA ZA KULEVYA.

08 Barabara ya Kivukoni, S.L.P. 80327, 11486 Dar es Salaam; Simu: +255 22 211 3754/57;
Nukushi: +255 22 211 3752; Barua pepe: cg@dcea.go.tz; Tovuti: www.dcea.go.tz